# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
## CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021** **KISWAHILI**

**(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

**Muda: Saa 3** **06 Novemba 2002 Asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali YOTE katika sehemu A, B, C na D na maswali MAWILI (2) kutoka sehemu E. Swali la 12 ni la lazima.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.
5. Mashine za hesabu za eletoni haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (ALAMA 10)

### UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika karatasi ya kujibia.

Dawa takriban za aina zote huathiri miili yetu inavyofanya kazi, hivyo hatuna budi tuzitumie kwa uangalifu. Matumizi mabaya ya dawa husababisha athari mbaya kwa mtumiaji. Aghalabu, matumizi mabaya ya dawa husababisha matatizo shuleni, nyumbani na kwingineko kwani mtumiaji anaweza kuvunja sheria za jamii na za nchi.

Aidha dawa haramu kama vile bangi, kokeini na heroini ni hatari zaidi kwani hutumiwa vibaya bila kuzingatia ushauri wa kitaalamu na hivyo kusababisha athari zaidi na hata kuleta maambukizi ya magonjwa kama ukimwi.

Matumizi ya dawa yanaweza kuwa ya muda mfupi au mrefu na athari zake hutokea kwa watumiaji wote. Baadhi ya watu hutumia dawa maisha yao yote, hususan wenye magonjwa ya muda mrefu kama kifafa, kisukari, mtindio wa ubongo na kadhalika.

Matumizi mabaya ya dawa ni yale yasiyolenga kuboresha afya ya mtu iwe kwa makusudi au kwa kutoelewa taratibu za utumiaji na hivyo kuleta madhara makubwa kwa mtumiaji. Mathalani mtu anatumia dawa bila kushauriwa na wataalamu au anagawa dawa zake kwa mgonjwa mwingine bila kufuata vipimo vya kitaalamu.

Pombe ni kinywaji ambacho kama kikitumiwa vibaya huleta athari kubwa kama ilivyo katika matumizi mabaya ya dawa. Mathalani mtu aliyelewa kupita kiasi hushindwa kujimudu na hivyo huweza kusababisha vurugu, ajali sambamba na mtumiaji wa dawa kama bangi, kokeini na heroini.

Dawa, siku zote ni nzuri kama zitatumika kwa malengo mazuri na kufuata vipimo na ushauri wa wataalamu. Wataalamu hawana budi kuwaelimisha watumiaji faida na hasara za kila dawa wanayotumia, vinginevyo dawa tunazotumia nyingi ni muhali kwa afya zetu. Suala la msingi la kuzingatia ni kwamba dawa hazipo kwa ajili ya kuburudisha watu bali kwa matibabu ya watu. Hivyo, tuwe makini kwa hili kwani mzaha mzaha mwisho ni usaha.

**MASWALI**

(i) Kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu hiki ni

A Matumizi ya dawa
B Faida za dawa
C Athari za pombe na dawa za kulevya
D Dawa zetu
E Dawa za kulevya.

(ii) "Dawa tunazotumia nyingi ni muhali kwa afya zetu". Maana yake ni

A dawa zinatosheleza haja ya afya zetu
B dawa zenye kutokubaliana na afya zetu
C afya za binadamu lazima ziboreshwe kwa dawa
D dawa za kulevya ni hatari kwa afya zetu
E dawa tunazotumia ni zenye hali nzuri kwa afya zetu.

(iii) Neno "aghalabu" katika kifungu hiki limetumika kama

A hususan
B kwa kuwa
C angalau
D mara nyingi
E hatuna budi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(iv) Mwandishi ana maana gani anaposema "Mzaha mzaha mwisho usaha"?

A Dawa zinaweza kuleta usaha mtu akizidiwa
B Tusiweke dawa karibu na watoto
C Tuwe makini na matumizi ya dawa
D Tusichezee pombe
E Hatuwezi kufanya dawa kama kiburudisho.

(v) Matokeo ya matumizi mabaya ya dawa ni

A kisukari, kifafa na kifua kikuu
B utumiaji wa bangi, heroini na kokeini
C kupenda anasa za dunia
D watu kutoacha pombe, heroini na bangi
E watu kupata matatizo shuleni, nyumbani na katika jamii.

(vi) Sababu kuu ya watu kutumia dawa ni

A kujiburudisha wao wenyewe
B kupunguza matatizo shuleni
C kujitibu wanapopata matatizo ya afya
D kurefusha maisha wanapokaribia kufa
E kuzitumia dawa kwa uangalifu zisidhuru afya.

(vii) Kwa ujumla aya ya kwanza katika kifungu hiki inaelezea nini?

A Dawa zote ni haramu
B Dawa zote ni kwa ajili ya watu
C Utumiaji wa dawa uendane na sheria za shule na za jamii
D Dawa zote zina uwezo wa kuathiri afya zetu
E Dawa za kulevya ni hatari kuliko dawa nyingine zote.

(viii) Neno "takribani" katika kifungu hiki maana yake ni

A karibu
B mara kwa mara
C ambapo
D ingawaje
E ingekuwa.

(ix) Mwandishi anatuasa nini katika kifungu hiki?

A Dawa zote ni nzuri
B Mazoea hujenga tabia
C Dawa zitumike kwa uangalifu
D Dawa zichunguzwe na Mkemia Mkuu kabla ya kutumika
E Watu wengi hawafahamu kutumia dawa wanazopewa.

(x) Mwandishi anadokeza nini juu ya pombe?

A Ina masharti magumu kwa watumiaji
B Ni chanzo kikuu cha uzembe
C Haifai kwa madereva wote
D Ni kiburudisho cha watu wengi
E Huweza kuleta madhara kwa watu mbalimbali.


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha andika ufupisho wa maneno hamsini (50).

Wanangu, tangu zamani bara letu la Afrika lilikuwa na mambo yaliyohitilafiana na haya tunayoyaona sasa. Hadithi, mikasa, vitimbi na visa vilivyotokea zamani katika sura ya nchi yetu vinatofautiana sana na nchi yoyote nyingine. Vyetu ni vitamu na bora kuliko vyote vile vilivyotokea katika nchi nyingine yoyote ile iwayo.

Miujiza ya mambo yaliyotokea ina mizizi ambayo viini vyake hubenua waziwazi mila na desturi za asili tangu zamani, hivyo hadithi hizo zina tija ya makumbusho ya daima milele. Kwa hiyo, katika hali yoyote yatupasa kuhifadhi hazina za mila zetu. Mila zetu zidumishwe; kwa mfano watu kuzunguka moto huku kizee kikongwe au ajuza akisimulia hadithi za mambo ya kale liwe ni jambo la kawaida kabisa.

Katika dunia ya leo simulizi hizo za ujasiri na uzalendo zimeenea kutoka vizazi hadi vizazi. Mambo mengi yamebadilika kutoka mitindo aina aina, hivyo mabadiliko hayo yasitufanye sisi kusahau simulizi zetu katika mitindo yetu. Ni wajibu utupasao kuendeleza tabia hizi ili tubenue mbinu za masimulizi hata kwa vitabu.

## SEHEMU B (Alama 20)

3. Chunguza kwa makini orodha **A** na **B** kisha eleza maana ya vifungu vya maneno katika orodha A kwa kutumia orodha **B.**

**ORODHA A**

(i) Wamewaibia
(ii) **za Kilimanjaro** nzuri zaidi
(iii) **u** mtoto wa mzee Sungura
(iv) Jioshe
(v) Mnyambuliko

**ORODHA B**

A Uambishaji wa maneno
B Kishazi pekee
C Kiwakilishi
D Kitenzi kishirikishi
E Oneshea
F Kiwakilishi cha a-unganifu
G Kiambishi cha nafsi ya pili wingi
H Agizo
I Kitenzi
J Mnyumbuliko

4. Sentensi zifuatazo ni tata. Toa maana mbili ili kuthibitisha utata huo.
(a) Juma amenunua mbuzi
(b) Ile nyumba ya wageni
(c) Yeye aliwachezea wanangu
(d) Mzee ameijia fedha yake
(e) Unaweza kuimba babu alimwuliza mtoto.

5. Andika insha yenye maneno 100 kuhusu moja ya mada zifuatazo:
(a) Mtu ambaye natamani kuonana naye
(b) Mcheza kwao hutuzwa
(c) Siku ya wapendanao.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (Alama 20)

## SARUFI

6. Kwa kutumia mifano, eleza kwa ufupi maana na aina tatu za tungo.

7. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya jedwali:
   (a) Dada mmoja ameleta kanga nzuri
   (b) Babu zetu walikuwa wanapiga ngoma zao vizuri.

8. Ainisha maneno katika sentensi zifuatazo:
   (a) Wanafunzi hodari hufaulu mara kwa mara
   (b) Kucheza kwao sikupendi tena
   (c) Hivi ataandika barua mapema?
   (d) Paka na panya ni maadui
   (e) Nilipolilipua likalipuka lip!

9. Nominisha vitenzi vifuatavyo
   (a) Hujumu
   (b) Azimia
   (c) Sifu
   (d) Tubu
   (e) Tangaza
   (f) Kufa
   (g) Dunda
   (h) Tambika
   (i) Lia
   (j) Zindika.

## SEHEMU D (Alama 10)
## HISTORIA YA LUGHA

10. Andika mambo muhimu manne (4) yanayopatikana katika maana ya lugha na kisha uyafafanue.

## SEHEMU E (Alama 40)
## FASIHI

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii. Swali la 12 ni la lazima.

11. Jadili athari zinazoikumba fasihi simulizi iliyohifadhiwa katika maandishi.

12. "Ukosefu wa elimu katika jamii hurudisha maendeleo ya jamii nyuma". Jadili kauli hiyo kwa kutumia vitabu viwili vya tamthiliya ulivyosoma kati ya hivyo vilivyoorodheshwa hapo chini.

13. "Miongoni mwa kazi za fasihi ni kuweka wazi maovu yaliyofichika na kuyakemea". Chagua washairi wawili kati ya walioorodheshwa hapo chini na jadili jinsi walivyotekeleza wajibu huo.

14. "Mwanamke anaonekana kama kiumbe dhaifu katika kutetea haki zake". Jadili hoja hii kwa kutumia vitabu viwili vya riwaya ulivyosoma kati ya hivyo vilivyoorodheshwa hapo chini.

**USHAIRI**

Diwani ya Mloka - C. Mloka (B.P)
Diwani ya Ustadh - A. Andanenga (B.P)
Malenga Wapya - Takiluki (DUP)

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**RIWAYA:**

| | | |
|---|---|---|
| Hiba ya Wivu | - | Z. Mwanga (R.P) |
| Kusadikika | - | S. Robert (Nelson) |
| Zawadi ya Ushindi | - | B. Mtobwa (R.P) |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| Hawala ya Fedha | - | A. Lihamba (TPH) |
| Mfalme Juha | - | F. Topan (DUP) |
| Ngoswe – Penzi Kitovu cha Uzembe | - | E. Semzaba (ESC) |

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org